**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Dodoma 12 Novemba 2025

**KIKAO CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI**

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania inapenda kuuarifu umma kuwa itafanya kikao cha Baraza la Wafanyakazi tarehe *18 na 19.novemba 2025* katika **Hoteli ya Sanaan**, iliyopo jijini Dodoma.

Kikao hiki kitawakutanisha Menejimenti ya Tume pamoja na wawakilishi wa wafanyakazi, wakilishi wa TUGHE ngazi ya Taifa na Mkoa na watoa mada maarufu hapa nchini kwa lengo la kujadili masuala muhimu ya kiutendaji, ikiwa ni pamoja na:

- Kuboresha mazingira ya kazi na ustawi wa watumishi;
- Kupitia utekelezaji wa mpango wa mwaka unaoendelea;
- Kujenga uelewa wa pamoja kuhusu majukumu ya Tume katika kusimamia na kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya sheria;
- Kuimarisha ushirikiano kati ya Menejimenti na Wafanyakazi ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa umma.

Tume inaendelea kuthamini mchango wa watumishi wake katika kutekeleza majukumu ya kitaifa ya kupitia na kupendekeza maboresho ya sheria mbalimbali nchini.

Imetolewa na:

**Bashiri S. Juma**
**Kitengo cha Mawasiliono Serikalini**

***Chuo Kikuu cha Dodoma,Barabara ya Mkalama,Jengo la Taaluma Na.1,S.L.P. 1718, Dodoma.***
***Tovuti: www.lrct@lrct.go.tz; Barua pepe: lrct@lrct.go.tz; Simu: +255734 356685/6***